

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



Unapojobu tafadhali taja;

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
4, Barabara ya Bomanji,  
S.L.P. 20,  
**21402 MUHEZA-TANGA**

Kumb. Na.HW/MUH/ S.80/113/207

07/03/2024

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

### 1: MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma Sura ya 298 za mwaka 2022 kifungu cha 110 na 111(4) (a) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kutuma maombi ya nafasi ya **Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira** kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2024 hadi 2028.

### SIFA ZA MWOMBADI

1. Awe Mtanzania.
2. Awe mkazi wa Wilaya ya Muheza.
3. Awe na Elimu ya ngazi ya **Stashahada ya juu** (Advanced Diploma) au **Shahada** ya kwanza na kuendelea katika fani ya **Utawala au Usimamizi wa Rasilimali** watu au **Sheria**.
4. Awe na umri wa kuanzia miaka 45 na kuendelea
5. Awe na uzoefu katika masuala ya Utawala au usimamizi wa Rasilimali Watu au Sheria.
6. Asiwe mtumishi wa Umma.

### MAJUKUMU YA KAZI

1. Atakua ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.
2. Kuongoza vikao vyote vya Bodi vinavyohusu Ajira kwa kufuata Kanuni, Sheria, Taratibu na Miongozo iliyopo.
3. Kuthibitisha watumishi Kazini, Upandishwaji wa Vyeo kwa watumishi na kubadilisha Vyeo watumishi kulingana na Miundo ya Utumishi wa Umma.

## **MASHARITI YA JUMLA**

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe mkazi wa Wilaya ya Muheza.
2. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la Jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, ya waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**)
4. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti nya taaluma, vyeti nya Elimu (Kidato cha IV/VI), Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU/NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
6. Waombaji waliostaafu/waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma wanaruhusiwa kuomba.
7. Hakutakuwa na mashahara kwa mwezi isipokuwa atalipwa posho ya vikao kwa kila kikao kitakapofanyika.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahuksika watachukuliwa hatua za kisheria.
9. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 20/03/2024 saa 9:30 Alasiri
10. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta au barua pepe au kupitia Masjala kuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa Anwani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA,**

**S.L.P. 20,**

**21402 MUHEZA TANGA**

Barua pepe: ded@muhezadc.go.tz

  
Edward Mgaya

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MUHEZA**

  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
MUHEZA**

**Nakala** Mbao za matangazo

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza